# Kazi za kukusaidia kujifunza ukiwa nyumbani na mtoto wako asiye na uwezo wa kusikia

Tengeneza mazingira ambayo mtoto wako anaweza kujifunza mwenyewe. Muonyeshe mtoto wako namna ya kunawa mikono kwa usahihi na pia jaribu kumueleza ni kwa nini kunafanya hivyo, ni muhimu kama vile angejifunza kutoka kwenye kitabu.

Zipo njia nyingi muhimu za kumfundisha mtoto stadi za Maisha:

› Kuhesabu vitu na kuonyesha namba kwa kutumia vidole vyako

› Kumueleza mtoto wako aina ya viungo ulivyoweka na namna vinavyobadilika wakati wa kupika

› Kumtajia mtoto wako majina ya miti, vilima, mito ya maji, matunda, mbogamboga, wanyama na ndege na kisha kujadili na kukubaliana alama za hivyo vitu. Au kuelezea, kushika, kuonja au kunusa vitu hivyo ili kuweza kujifunza rangi, maumbo, ladha, harufu na muundo

› Kumsaidia mtoto wako kuchagua herufi kutoka kwenye jina lake


› Kuwafundisha kutaja muda


# Mazoezi mbalimbali ya watoto wadogo viziwi na waisio na uziwi ambao wanajifunza nyumbani

## Maonyesho ya vipaji

Chora kitu au mnyama yoyote kwenye karatasi au chini kwenye mchanga. Unaweza kutumia picha kutoka kwenye magazeti au picha maalumu kama unazo. Chora kitu hicho kama mara nne au tano. Wakati wa kuchora picha jitahidi zote zifanane lakini jaribu kubadilisha vitu vichache. Mfano; kama unachora picha ya mbwa au tembo, jaribu kuchora mmoja akiwa na mkia mrefu na wengine wakiwa na mikia mifupi.

- Je, masikio yamefanana?
- Je, ni lipi liko tofauti?
- Je, yote yana ukubwa sawa?





## Mkiwa pamoja tena mfanye yafuatayo

Chora picha yoyote ya kawaida au tumia ambayo umetoa kwenye gazeti. Kata na tenganisha picha hiyo kwenye vipande kadhaa, kisha muombe/mwambie mtoto wako ajaribu kurudishia/kuunganisha vipande vya picha hiyo kama ilivyokuwa mwanzo – kama vile mchezo. Au chora picha ya paka au mnyama yoyote kisha kata kipande kutoka katika picha hiyo, kisha muombe/mwambie mtoto ajaribu kuchora sehemu/kipande cha picha hiyo iliyotolewa.



# Mazoezi kwa ajili ya watoto wadogo wanaojifunzia nyumbani

## Vitu vinavyokosekana

Kusanya vitu mbalimbali vilivyoko mazingira ya nyumbani na uviweke pamoja. Kisha muuliza mtoto wako aviangalie vitu hivyo na kuvitaja majina yake. Mwambie afumbe macho au aangalie upande mwingine au nyuma, toa kitu kimoja wapo, kisha mwambie aangalie tena na muulize kama ana kumbuka ni kitu gani ambacho hakionekani. Unaweza kulifanya zoezi hili kuwa gumu kidogo kwa kuongeza vitu vingine zaidi. Ni mchezo mzuri ambao unaweza kuufanya kwa kubadilishana na mtoto wako, pindi anapotoa kitu chochote na wewe kuweza kukisikia ni kitu gani ambacho hakionekani. Mazoezi haya yatakusaidia wewe pamoja na mtoto wako kuweza kuwasiliana na kuwasaidia kujifunza maneno na alama mpya.

## Kutaja majina ya vitu

Hii ni njia nzuri ya kumsaidia mtoto kuoanisha/kufananisha maneno, alama pamoja na vitu. Pia unaweza kuwa na maneno ya kuelezea sifa za kitu; mfano kiti kidogo, meza kubwa, taa ya bluu. Jaribu kuonyesha alama au kwa ishara kama hujui lugha ya alama sahihi ya maneno hayo. Au kama mtoto wako kiziwi anajifunza lugha ya alama shuleni muulize akuonyeshe alama husika ya maneno hayo. Kama mtoto wako yuko tayari kuanza kujifunza kusoma na kuandika, mpe zoezi la kuandika vikaratasi vyenye majina ya vitu vilivyoko nyumbani na kuviweka katika vitu hivyo. Hili litamsaidia kufanya mazoezi ya kujifunga kuandika, kutamka na kuandika herufi na kujifunza maneno mapya.

## Kulinganisha nambari

Chora maduara nje kwenye mchanga au kwenye karatasi na kisha andika nambari kuanzia 1 hadi 10 kwenye kila duara. Kusanya na weka pamoja vitu mbalimbali (mfano; vifuniko vya chupa, mawe, karanga) na kisha mpe zoezi mtoto wako la kuweka idadi kamili ya vitu katika kila duara. Zoezi hili litamsaidia mtoto kiziwi kuweza kulinganisha majina ya nambari, maumbo yake, kuhesabu kwa umakini na kujifunza maneno mapya katika njia ya michezo.

## Kuigiza

Tumia mdoli kuigiza kazi za kila siku. Kupitia zoezi hili watoto wanaweza kujifunza majina na alama za viungo vya mwili na kazi zingine. Labda pia mdoli anaweza saidia katika kujifunza kupika, namna ya kuvaa nguo au majukumu na kazi zingine.

# Kazi na mazoezi ya watoto wakubwa na wadogo wasio na uwezo wa kusikia ambao wanajifunza wakiwa nyumbani

**Kulingana na umri na madarasa waliyopo, watoto wasio na uwezo wa kusikia wanaweza kuwa na vitabu vya kujifunzia, lakini hata kama hawana wanaweza kuendelea kujifunza pindi wakiwa nyumbani. Kama kuna upatikanaji wa mtandao/intaneti unaweza kutumia tovuti au programu mbalimbali za mtandaoni ambazo zinaweza kusaidia wao kujifunza, lakini ni lazima kuwa makini kuhakikisha tovuti hizi ni salama na mtoto hatumii kifaa hicho muda mrefu. Walimu na wadau wengine waliopo jirani na maeneo yako wanaweza kujua tovuti nzuri za kujifunzia na pia unaweza kuwauliza kutoa maoni yao juu ya hizo tovuti.**

## Alama na Ishara

Muombe mtoto wako akufundishe alama mbalimbali ili uweze kujifunza na kuwasiliana nae zaidi. Hili linaweza kufanyika kama mashindano au mchezo katika familia na kuangalia ni nani ameweza kujifunza alama nyingi zaidi, lakini pia kumbuka kujua alama za vitu ni mwanzo/hatua za kwanza za kujifunza Lugha ya Alama.




## Kutumia vitabu

Kama mtoto wako amerudi nyumbani na vitabu vya shule, mpe moyo na msaidie aweze kusoma vitabu hivi. Kuna mazoezi katika vitabu ambayo unaweza muelekeza mtoto akajaribu kuyafanya. Ni vizuri pia mtoto akawa na daftari akaandika majibu. Zingatia na fuatilia mazoezi wanayoyafanya, jadili pamoja nao na wasaidie katika mazoezi hayo; sahihisha kazi zao kama unaweza. Au kama wana ndugu mkubwa anaweza kusoma nao au akawa kama mwalimu.



## Kushiriki katika kujifunza pamoja na ndugu (kaka, dada au ndugu wengine)



Watoto wakubwa wanaweza kushiriki katika kuwafundisha watoto wadogo kusoma, kuandika na kuhesabu. Wanaweza kuwachangamsha watoto wadogo kwa kuwaambia hadithi mbalimbali au kuwachora kwenye karatasi au chini kwenye mchanga. Wanaweza kutengeneza mchezo na kuweka sheria namna ya kucheza, kisha kufundisha mchezo huo kwa watoto na watu wengine katika familia.



# Mazoezi kwa ajili ya watoto wakubwa na wadogo wasio na uwezo wa kusikia wanaojifunza wakiwa nyumbani

## Mazoezi mengine ya ajili ya kujifunza

Watoto wakubwa wasio na uwezo wa kusikia wanaweza kusaidia katika kuandika orodha ya vitu vya kununua na kisha kufanya mchanganuo wa fedha inayohitajika kununua vitu hivyo. Zoezi hili litamsaidia kujua kuandika na kufanya hesabu. Au kama huwezi kuondoka nyumbani unaweza kutenga chumba au sehemu ndogo na kupafanya kama duka au meza ya sokoni ikiwa na vitu vichache vya kuuza. Mtoto anaweza kuigiza kama ananunua vitu na kuvilipia au wanaweza kuigiza wao ni wauza duka wakajaribu kuhesabu hela na kutoa chenji baada ya malipo. Kupitia zoezi hili la ununuzi wa vitu watoto wanaweza kujifunza masuala yahusuyo fedha.

Waombe wakuambie hadithi yoyote, na kama unaweza andika hadithi hii. Wanaweza kukuambia kuhusu shule, mchezo wanaoupenda au kumuelezea mtu wanaemfahamu. Vinginevyo, wanaweza kuandika chakula, viungo vyake na maelekezo ya namna ya kupika au hata kushiriki katika kusaidia kupika.

Kwa wale ambao bado wanajifunza kuandika, wape zoezi la kuandika herufi na maneno, kila mara jaribu kuwasaidia kuelewa maana ya neno na si tu kujua kuliandika. Toa alama au ishara kama bado hufahamu vizuri au muulize mtoto akufundishe alama ambazo ameshajifunza.

### Mti wa Familia

**(Mchoro wa mti unoelezea uhusiano wa ndugu katikafamilia)**

Fanya zoezi hili na mtoto wako kwa kuchora mti wa familia ukionyesha uhusiano uliopo kwa wanafamilia.

### Ramani

Fanya zoezi na mtoto wako la kutengeza/kuchora ramani ya mahali/mtaa mnapoishi mkionyehsa barabara, majengo, mashamba, maduka, shule n.k. Toa taarifa/maelezo yanayojitosheleza.

Chunguza namna mbegu zinavyoota na kuwa mimea kwa kuangalia maua, miti na vichaka viliyoko nyumbani. Muonyeshe mtoto wako picha yoyote ya sikukuu na kisha jadili mambo yanayofanyika katika picha hiyo. Fikiria ni nini huwa kinatokea na kufanyika kipindi cha sikukuu hiyo na lini huwa inafanyika katika kalenda.

**Kujifunza pamoja na mtoto wako asiye na uwezo wa kusikia ni jambo linaloweza kuwa la kuchangamsha na kufurahisha! Jifunze na tafuta njia bora za kuwasiliana PAMOJA.**